**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA**

**JIMBO LA BUCHOSA**

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MUDA YA UCHAGUZI WA MARUDIO YA UDIWANI KATA YA NYAKASUNGWA JIMBO LA BUCHOSA

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 6 (6) na 76 vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani na 1 ya mwaka 2024 na kwa maelekezo ya Mkurugenzi wa Uchaguzi, Wasimamizi wa Uchaguzi wanatakiwa kuteua Watendaji kwa idadi inayohitajika kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika Kituo cha Kupigia kua Watendaji ambao watateuliwa katika Kituo ni Wafuatao:-

i. Wasimamizi wa Kituo vya kupigia Kura
ii. Wasimamizi wa Kituo wa akiba
iii. Wasimamizi wa Wasaidizi wa Kituo
iv. Karani muongozaji wapiga kura
v. Makarani waongozaji wapiga kura wa akiba.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

1. Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia maika 18 na kuendelea;
2. Awe na Elimu isiyopungua kidato cha nne;
3. Awe mwaminifu, mwenye maadili na asiye na rekodi ya makosa ya jinai;
4. Asiwe Mwanachama wa chama chochote cha Siasa;
5. Awe tayari kufanya kazi kwa muda wote uliopangwa bila urasimu;
6. Awe mkazi wa eneo husika au maeneo ya jirani yatakayoruhusu kutekeleza majukumu kwa ufanisi.

Waombaji wanapaswa kuwasilisha maombi yao kwa maandishi yakifuatana na nakala zifuatazo **cheti cha Elimu, Kitambulisho cha NIDA, Kitambulisho cha Mpiga Kura pamoja na Leseni ya Udereva.**

**Maombi yote yawasilishwe OFISI YA MTENDAJI WA KATA AYA NYAKASUNGWA kabla ya tarehe 25.11.2025 saa 10:00 Jioni maombi yatakayowasilishwa baada ya muda huu hayatazingatiwa.**

Tangazo limetolewa na:-

Deogratias C. Lihengelimo
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**
**JIMBO LA BUCHOSA**
20 NOVEMBA, 2025

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
JIMBO LA BUCHOSA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUC...

S.L.P 44, BUCHOSA-SENGEREMA, Simu+255 (026) 2963630,Nukushi +255 (026) 2963629,
Baruapepe: ded@buchosadc.go.tz, Tovuti: www.buchosadc.go.tz